

Public education  
Discover a world of opportunities

# SAYANSI: KUSOMEA NYUMBANI

## SAYANSI KATIKA BUSTANI

### Kuchezea namaji

- Mfanye watoto wako kufikiri maji yanatoka na inenda wapi. Pima mawazo yao kwa kuwataka wapake rangi au dawa ya maji kwenye uso halisi na kuangalia maji yanavyotoweka.
- Zungumza jinsi unyevu unavyokauka.
- Safisha gari. Ruhusu mtoto wako kusikia nguvu ya maji kutoka kwenye mbomba. Tengeneza povu na sabuni. Uliza maswali kama vile: *Maji na uchafu zinaenda wapi?*
- Weka upande mmoja wa kitambaa cha mkono katika maji na kuondoka upande wa pili juu ya ardhi. Angalia kiwango cha maji katika bakuli baada ya dakika tano na kuuliza mtoto wako maswali kama: *Kiasi gani cha maji kimebakii katika bakuli? na kwa nini hiyo inafanyika?*

### Mwezi

- Angalia mwezi kila siku kwa mwezi mzima. Uliza watoto wako kuchora mchoro wao wanavyo tazama mwezi na zungumzia kuhusu jinsi mabadiliko ya sura yanatokea kutoka usiku kwa usiku. Wafanye wakueleze sura, kwa mfano: *mpevu, robo, nusu na kamili*. Tafuta kujua ni siku ngapi inachukua kati ya mwezi mmoja kamili na mwagine.
- Tumia darubini na kuuliza watoto wako kuchukua zamu kuangalia wenyewe na wafanye wakueleze mwezi kwa undani zaidi, kwa mfano sura ya nje.



Department of  
Education

**Utapa zaidi**  
**Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani**  
**Elimu hapa: [education.wa.edu.au](http://education.wa.edu.au).**